

Bei iliopunguzwa kwa malipo juu ya huduma katika chekechea na shule za utunzaji wa mchana (utunzaji asubuhi kabla shule kuanza na baadaye shule kuisha) SFO kwa ufupi.

Bei katika chekechea na shule za matunzo ya baadaye shule kufunga hayiwezi kuzidi kiasi cha asilimia 6% ya mapato binafsi na mapato ya mtaji ya kaya kwa kila mtoto. Ikiwa bei imezidi asilimia 6 %, unaweza kutuma maombi ya kupunguzwa kwa malipo ya wazazi. Hii maana yake ni kwamba familia zenye kipato/ mapato kidogo zinaweza kupunguziwa na kulipa kidogo sana katika chekechea na SFO.

Kwa mapato ya kibinafsi na ya mtaji ya kaya yanayotozwa ushuru, tunamaanisha wenzi, wenzi waliosajiliwa na wakaaji wenza wanaoishi kwa anwani pale ambapo mtoto amesajiliwa.

Ikiwa mtoto ana makazi sehemu mbili, malipo kwa wazazi yatahesabiwa kulingana na mapato ya mzazi mwenye anwani sawa na mtoto kwa rejista ya raia.

Manispaa ya Bergen ina vikomo tofauti vya mapato/mipaka na mipango ya malipo yaliyopunguzwa.

Tunapunguza bei yako kulingana na bei ya juu ya sasa katika shule chekechea na SFO, mapato ya kaya na umri wa mtoto. Manispaa ya Bergen ina mipango mbalimbali ya malipo yaliyopunguzwa. Unaweza kusoma zaidi kuhusu vikomo vya mapato na mipango mbalimbali inayoathiri bei yako ya shule chekechea na SFO hapa (kwa Kinorwe pekee):

<http://www.bergen.kommune.no/reduisert-foreldrebetaling>

Unapata punguzo ya wandugu ikiwa una watoto kadhaa wanaoenda shule chekechea / SFO, bila kujali mapato ya kaya.

Ni lazima utume ombi la kupunguziwa malipo

Fomu ya maombi inaweza kupatikana hapa: <http://www.bergen.kommune.no/reduisert-foreldrebetaling>

Maombi ni ya kielektroniki na lazima uwe na Kitambulisho cha Benki, Kitambulisho Changu au kitu kama hicho ili utume ombi.

Ikiwa una watoto wengi, lazima utume ombi kwa kila mtoto katika programu sawa. Hesabu basi inafanywa kiotomatiki katika programu yako.

Ili tuweze kupata bei yako ya huduma ya kulelea watoto kwa chekechea na baada ya shule ya mchana na kushughulikia ombi lako, ni lazima uambatishe hati halali za mapato yanayotozwa kodi ya kaya:

- Marejesho ya hivi karibuni ya ushuru
- Iwapo kuna mabadiliko makubwa na ya kudumu katika mapato kuhusiana na marejesho ya kodi, unaweza kuambatisha hati za malipo ya mshahara ya miezi tatu ya mwisho.
- Uamuzi wa msaada kutoka kwa mfuko wa mkopo na cheti cha mwanafunzi
- Uamuzi kutoka kwa NAV
- Ikiwa unasubiri ufafanuzi kutoka NAV, lazima uambatishe na hati hii

Iwapo wewe umefika na ungali mupya nchini Norway na huna fomu ya kurejesha kodi, ni lazima uambatishe hati za ukaaji halali nchini Norway.

Ombi linahusu wakati gani?

Ombi la kupunguzwa kwa malipo ya wazazi inatumika kuanzia mwezi baada ya maombi kupokelewa. Tutakutumia uamuzi wakati ombi limeidhinishwa.

Ikiwa huna nambari ya hifadhi ya jamii au huwezi kutuma ombi kwa njia ya kielektroniki Huduma ya Raia inaweza kukusaidia kutuma ombi,

Nambari ya simu ni 55 56 55 56. Anwani ni Kaigaten 4.

Leta kitambulisho halali na nyaraka kwa maombi baada ya kuhudhuria.

NB! Kumbuka kutuma ombi ya chekechea / SFO kwa kila mwaka

Maamuzi kuhusu malipo yaliyopunguzwa ya mzazi yanatumika kwa mwaka mmoja kila wakati. Ni lazima utume ombi jipya kabla ya Julai ili uweze kupokea malipo yaliyopunguzwa mnamo mwezi wa mnane /agosti.